Chuka University
info@chuka.ac.ke | 020 231 0512 / 020 231 0518

# UHALISIA WA KIMANDHARI NA KIMAUDHUI KATIKA RIWAYA YA SIKU NJEMA (1996)

***Dorcas M Musyimi*[1], *Mary K. Njeru*[2]**
*Chuo Kikuu Cha Chuka, Anwani: Box 109-60400, Chuka. dmusymi@chuka.ac.ke;*
*mnjeru@chuka.ac.ke, 0723-479 668*

**How to cite:**
Musyimi D. M., & Njeru, M. K. (2021). Uhalisia wa kimandhari na kimaudhui katika riwaya ya siku njema (1996). In: Isutsa, D. K. (Ed.) *Proceedings of the 7th International Research Conference held in Chuka University from 3rd to 4th December 2020, Chuka, Kenya*, p.435-442

**ABSTRACT**
According to Ntarangwi (2004), literature portrays in a wider way the realism of the society. In addition, he states that one function of literature is to help human beings to bring out personal and society's challenges. It is a tool that helps human beings to understand themselves and their environment. Therefore, this paper aims to highlight the environmental and thematic realism in the *Siku Njema (1996*) story book. The paper has applied the Realism Theory in order to bring out the environmental and thematic realism. The data used was collected by reading the selected text then analysed according to the research objective and the theory tenets. The results indicate that the environment and the themes discussed in the selected text are real because the environmental place names used by the writer are found in real places in Uganda, Tanzania and Kenya. In addition, the themes highlighted by the writer have a close relation with the challenges the present society is facing. The writer seems to have been influenced by his immediate environment and happenings. This is an indicator that his work has not been created from a vacuum hence literature is a true picture of the society.
**Keywords:** Realism, Environment, Themes.

**IKISIRI**
Kulingana na Ntarangwi (2004), fasihi huwakilisha maisha kwa upana wake na hasa uhalisi wa kijamii. Aidha, anasema kuwa mojawapo ya majukumu muhimu ya fasihi ni kuwasaidia wanadamu kuyaeleza vyema masuala wanayokumbana nayo kibinafsi na pia kama jamii. Isitoshe, fasihi ni chombo kinachoisaidia jamii kujielewa na kuyaelewa mazingira yake. Basi, lengo la makala haya ni kubainisha uhalisia uliopo wa kimandhari na kimaudhui katika riwaya ya *Siku Njema (1996*). Makala haya yametumikiza nadharia ya Uhalisia ili kubainisha uhalisi uliopo wa kimandhari na kimaudhui katika riwaya husika. Data ya makala haya ilipatikana kwa kusoma riwaya husika kisha ikachanganuliwa kwa misingi ya malengo na nadharia teule. Matokeo ya uchunguzi yamethibitisha kwamba kuna uhalisi wa kimandhari na kimaudhui katika riwaya ya *Siku Njema* (1996) kwa sababu majina ya mazingira yanayozungumziwa na mwandishi yanapatikana katika Afrika Mashariki husasan nchini Uganda, Tanzania na Kenya. Isitoshe, maudhui yaliyoangaziwa na mwandishi yana ukuruba na masuala yanayoikabili jamii ya leo. Mwandishi anaonekana kuathiriwa na mazingira yaliyomzunguka pamoja na matukio ya jamii yake ya karibu. Hii ni ishara kuwa kazi yake haijabuniwa kutoka katika ombwe tupu. Dhihirisho kwamba, fasihi ni picha halisi ya jamii.
**Maneno Muhimu:** Uhalisia, Mandhari, Maudhui

## UTANGULIZI
Kulingana na Mushumbwa (2018), kile anachotunga mwanafasihi hukitoa katika mazingira ya jamii fulani ambayo yeye ni mhusika kwa namna moja au nyingine. Kazi yake ya fasihi anayoiumba msanii, hutokana na ufahamu wa msanii mwenyewe juu ya maisha na matukio ya jamii hiyo kutokana na kufahamu miktadha anuai ya jamii hiyo. Maudhui huyaumba kulingana na aina ya mipaka ya muktadha wa jamii anayoitungia kazi hiyo ya fasihi. Isitoshe, fasihi ni chombo kinachoisaidia jamii kujielewa na kuyaelewa mazingira yake. Basi, lengo la makala haya ni kubainisha uhalisia uliopo wa kimandhari na kimaudhui katika riwaya ya *Siku Njema* (1996) ikitiliwa maanani kwamba fasihi ni kielelezo cha hali halisi ya jamii.

**Wasifu wa Mwandishi Prof. Ken Walibora**

Kulingana na Cheruiyot (2020), Ken walibora alizaliwa Januari 6, mwaka 1964 kama mtoto wa tatu (kitinda mimba) wa Peter Wafula na Ruth Nasambu Makali na kuitwa jina la Kennedy Walibora Waliaula huko Baraki, kaunti ya Bungoma magharibi mwa Kenya, kisha wakahamia Kitale akiwa na miaka minne na baadaye Cherangany. Mamake aliaga 1984 akiwa miaka 51 kutokana na ugonjwa wa muda mrefu. Ken alikuwa na umri wa miaka 20. Naye babake aliaga mwaka wa 2006. Mwandishi alikuwa na majina mawili ya Kiingereza, Kenny na George. Alichagua kutumia jina Kennedy. Baadaye alibadili jina lake na kufahamika kama Walibora, ambalo lilikuwa linamaanisha kuwa ni bora kwa Kiswahili na kufupisha jina lake la kwanza kuwa Ken. Baada ya mamake kuaga, Ken alilelewa na mamake wa kambo Eunice Wafula.

Kulingana na tawasifu ya Ken Walibora katika riwaya ya *Nasikia Sauti ya Mama* (Walibora, 2014) inayoelezea maisha yake, walihama Baraki baada ya kifo cha ndugu yake ambaye inaaminika alitiliwa sumu na mke wa ndugu wa kambo wa babake. Baada ya kakaye Ken kufa na kuzikwa na matanga yakiwa bado hayajamalizika, yule muuaji alipania kumuua Ken Walibora ambaye alikuwa bado hajafikisha mwaka mmoja. Mtuhumiwa anakisiwa alienda akamchukua Ken kutoka kwa dadake ambaye alikuwa amempakata, akaenda naye nyuma ya nyumba na dadake kumfuata ambapo alishuhudia akimlisha kitu cha ajabu. Baada ya hapo, afya yake Ken ikadhoofika lakini kwa bahati nzuri akaokolewa na wataalamu wa kuganga matatizo ya aina hiyo.

Alipofikisha umri wa kwenda shule mwaka wa 1971 alijiunga na shule ya msingi ya St. Joseph. Ken alikuwa kisu butu darasani enzi hizo, kwani alipokuwa katika darasa la pili aliwahi kuvuta mkia kwa kuibuka namba sabini na mbili katika darasa la watu sabini na wawili katika mtihani wa mwisho wa muhula wa kwanza katika shule ambayo babake alikuwa mwalimu mkuu. Licha ya kukejeliwa na msichana mmoja aliyekuwa wakisoma naye darasa moja na ambaye alishikilia namba sita katika mtihani huo, familia yake haikumkejeli bali ilimtia moyo mamake akimwambia angefanya vyema muhula huo kwani hakuwa mjinga. Baada ya kuvuta mkia, aliongoza katika somo la uchoraji.

Kipindi hicho Ken alitamani kuwa vitu viwili akija kuwa mkubwa pamoja na moja aliyochaguliwa na babake. Alipenda kuwa polisi kwa vile alivyoona watu wakiheshimu polisi au labda kuwaogopa enzi hizo. Chaguo lake la pili lilikuwa kufanya kazi katika redio. Babake alikuwa miongoni mwa watu wachache waliomiliki redio kijijini. Majirani wakilazimika kuja kwao kila jioni kusikiliza matangazo. Chaguo la tatu na ambalo alikuwa amechaguliwa na babake ni kuwa mhandisi. Enzi hizo hakujua mhandisi ni nani lakini baada ya kufanya utafiti wa kitoto akabaini kuwa mhandisi ni fundi wa magari. Hakupendezwa na pendekezo la babake la kufanya kazi ambayo ingemlazimu kuvaa msurupwenye mchafu.

Ken akiwa darasa la tano alikuwa bado hajui kusoma ndipo mamake na kisomo chake cha darasa la nne kilichomfaa kusoma Biblia ya Kiswahili kwa kimaragoli akaamua kufanya kile ambacho walimu walishindwa kufanya katika miaka mitano Ken alipokuwa katika mikono yao na kwa kweli alifanikiwa. Ken akawa akimsomea mamake Biblia wakati ndwele zilimzidi akashindwa kusoma. Kujua kusoma kulimfanya ajue kiulizwacho kwenye mitihani na bila shaka akawa akijibu sahihi. Ken wa sufuri akaja vingine. Alipofanya mtihani wa darasa la saba alikuwa wa sita katika shule yao akiwa na alama ishirini na nne kwa thelathini na sita na kujiunga na shule ya upili Teremi karibu na Kamusinga. Gikambi (2020), anasema kuwa Ken alifariki tarehe 10 Aprili baada ya kugongwa na gari Nairobi kama polisi walivyoripoti. Alizikwa Jumatano tarehe 22 Aprili nyumbani kwake Makutano kwa Ngozi, jimbo la Cherang’any huko kaunti ya Trans Nzoia magharibi ya Kenya.

**Muhtasari wa Riwaya ya "*Siku Njema.*"**

Riwaya ya *Siku Njema* iliandikwa na Ken Walibora, 1996. Hadithi hii inamhusu Msanifu Kombo au Kongowea Mswahili aliye mhusika mkuu. Mwandishi ameangazia masuala ambayo ni halisi katika jamii ya sasa kama vile ukahaba, magonjwa, malezi ya watoto, matatizo yanayoikabili lugha ya Kiswahili, ndoa, uanaharamu, uadilifu, umaskini, matumizi ya dawa za kulevya na mabadiliko. Katika riwaya hii mhusika mkuu Kongowea Mswahili anapitia katika changamoto mbalimbali kama vile kuzaliwa na mamake Zainabu Makame na kukosa kufahamishwa kuhusu babake, mamake kufa na kisha kulelewa na Mjomba Kitwana pamoja na Mwana Saumu aliyemtilia sumu ili afe na kutafutwa na Selemani Mapunda ili amuue kwa kumsema kwa polisi baada ya kumfumania akimpiga hedimasta wa shule yao. Ilimbidi Kongowea kutorokea Mombasa kwa Mjombake Salim Makame ili Selemani Mapunda asimpate. Hata hivyo, alimfuata kule akiwa na nia ya kulipiza kisasi. Wanapopatana kisadfa, Kongowea anaamua kuhamia bara huko Kitale ili kumtafuta babake Juma Mukosi. Anapompata babake, anamwambia amtembelee. Kongowea anachelea na kumpata ashaaga. Kwa kufuata maagizo katika barua aliyomwachia chumbani anamzika na kurithi mali yake.

**Nadharia ya Utafiti**

Makala haya yametumikiza Nadharia ya Uhalisia. Nadharia hii iliasisiwa katika karne ya 19 na kufafanuliwa zaidi na E. Goffman aliyeishi kati ya mwaka (1922- 1982). Baadhi ya wataalamu wengine wanaotoa mchango wao ni Gustav Flaubert (1846-1854), George Lukacs (1963), Rene Wellek (1960), Macdowall Arthur (1918) na Hegel G. (1979). Lukacs (1963) anaeleza kuwa mwandishi anasukumwa na njia ya kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na wakati wake maalumu. Mwandishi anapaswa kupenya chini ya picha za kijuujuu na kudhihirisha mifanyiko ya mabadiliko yaliyopo. Uhalisia wa maisha katika jamii unapewa msingi mkubwa wa uandishi kuhusu uhalisia. Tukio, mhusika au mandhari huelezwa kama vya kihalisia ikiwa vinafanana na sura fulani ya maisha.

Naye Wamitila (2002) anaeleza kuwa uhalisia unasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Waandishi wa kazi teule wanatoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii ya mwandishi anayehusika. Fasihi yoyote lazima ionekane kama kioo cha jamii. Hivyo basi, lazima jamii iweze kujitazama na kujiona kupitia fasihi ambayo ni zao la jamii. Msingi wa nadharia hii ni kuwa sanaa iwakilishe ukweli na kuwakilishwa kwa maneno halisi, iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira. Nadharia hii imetumika ili kusaidia kubainisha jinsi mwandishi wa riwaya ya *Siku Njema* alivyoangazia mandhari ya kuaminika katika jamii yake. Pia, mwandishi anazungumzia matatizo yanayoikabili jamii katika uhalisia wake. Wahusika wake wanafanikisha katika kuyaelezea mambo haya.

## MBINU ZA UTAFITI

Data ya makala haya ilipatikana kwa kuipitia riwaya ya *Siku Njema* (Walibora, 1996) na kisha kuichanganua kwa kufuata mandhari yaliyotumiwa na mwandishi na maudhui yaliyoangaziwa.

### Uhalisia wa Mandhari na Maudhui katika *Siku Njema*

Baada ya kuipitia riwaya teule, mtafiti amegundua kuwa kunao uhalisia kuhusu mandhari na maudhui yaliyoangaziwa na mwandishi.

### Uhalisia wa Kimandhari

Kulingana na TUKI (2014), mandhari ni sura ya mahali na jinsi panapoonekana. Nayo mazingira ni hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu anapoishi au maisha yake. Kwa mujibu wa makala haya neno mandhari litatumika. Mandhari haya huweza kuwa halisi kama vile baharini, njiani, msituni, kijijini, mijini au ya kufikirika kama vile kuzimu, mbinguni na peponi. Mtunzi wa hadithi anaweza kutumia mandhari kuelezea mazingira halisi ya kisa anachosimulia. Pia anaweza kufikisha ujumbe wake kwa jamii husika kwa kutumia mazingira yanayoeleweka na wasomaji. Hivyo mandhari humsaidia msomaji kung'amua ujumbe akirejelea tukio husika. Ni kutokana na haya ambapo makala haya yanachunguza uhalisia wa mandhari ambayo yameangaziwa katika riwaya ya *Siku Njema*. Mwandishi Ken Walibora amefanikiwa katika kujenga visa na matukio katika mandhari halisi. Ametumia majina halisi ya miji inayopatikana katika nchi za Afrika Mashariki zikiwemo Kenya, Uganda na Tanzania.

### Mandhari ya Nchi ya Tanzania

Katika uk.1, mwandishi anasema kuwa Zainabu alizaliwa Mwanza 1927 kama mtoto wa tatu wa Mzee Mwinyi Makame. Kutokana na uhasama wa wake wenza, mamake Zainabu alihamia kijiji cha Chongoleani katika mkoa wa Tanga (uk 2). Zainabu alikuwa na kipawa cha uimbaji wa taarab ndiposa akajiunga na kikundi cha Mbelewele mjini Tanga. Pamoja na wenzake walitembea Dar es Salaam, Nairobi na Kampala. Msanifu Kombo alizaliwa Tanga 1957. Mjini Tanga ndiko Mjomba Kitwana alikokuwa na karakana ya kutengeneza majeneza. Watoto wa Kitwana: Butambo, Daniel na Rehema walisomea Tanga School pamoja na Msanifu Kombo, Vumilia, Selemani Mapunda na Amina. Ni katika Tanga School ambapo Msanifu alitunga hadithi kumhusu kijana Kongowea Mswahili na ikachukua nafasi ya kwanza katika mashindano ya uandishi katika shule mkoani Tanga ndiposa wanafunzi wakampagaza Kongowea Mswahili (uk 7).

Makazi ya Enock Minja mpwaye Mwana Saumu yalikuwa Tabora (uk 23). Amina anasema kuwa alizaliwa Dodoma (uk 55-56) na kuambatana na babake hadi Tanga alipokuwa akifanya kazi na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Dodoma ndiko Amina alikopatana na mchumbake Onyango aliyekuwa mwalimu wa Kiingereza katika shule ya Sekondari. Isitoshe, Amina anasema kuwa siku aliyobakwa na babake wa kambo, mamake alikuwa amekwenda kumtembelea kakake Sumbawanga. Tunaelezwa kuwa mhusika Mercy Macdonald aliwahi kufanya kazi katika hopsitali ya Muhimbili na kuishi mtaa wa Buguruni-Dar es Salaam (uk 109).

### Mandhari ya Nchi ya Uganda

Kongowea anapopatana na Amina akisafiri kwenda Mombasa, Amina anamwambia kuwa walisoma pamoja Tanga School kwa mwaka mmoja kwani babake alifanya kazi na Jumuiya ya Afrika Mashariki basi wakahamishwa kutoka Tanga hadi Kampala (uk 56). Mercy Macdonald anamwambia Kongowea kuwa aliwahi kufanya kazi katika hospitali ya Mulago mjini Kampala (uk 110).

### Mandhari ya Nchi ya Kenya

Nchini Kenya mwandishi amerejelea maeneo ambayo ni halisi na msomaji anayetoka humo anaweza kuyafahamu kwa urahisi. Kongowea alipopata habari kuwa Selemani alitaka kumuua kwa kumsema kwa polisi, Kitwana alimshauri kusafiri hadi Mombasa alikoishi mjombake Salim Makame (uk 43). Khamis alisema kwamba Salim

aliishi Kisauni Msikitini. Katika chombo cha usafiri, Kongowea alikutana na Amina. Wawili hawa walishukia Mwembe Tayari-Mombasa (51). Katika mazungumzo yao, Amina alimweleza Kongowea kuwa, asili ya mchumbake Onyango ilikuwa Ukwala (uk 56).

Kongowea alipofika Mombasa usiku, asubuhi alipanda basi katika kituo cha Kenya Bus Services ili kwenda kushukia Kisauni Msikitini (uk 60). Alipofika Kisauni, alipata kwamba Salim Makame alikuwa amenunua nyumba za kukodisha kule Mtwapa (uk 65) na aliyemkaribisha kwa mjombake ni mpangaji Rashid aliyefanya kazi katika Dolphin Hotel (uk 66). Bibiye Salim aliitwa Wamboi kutoka Murang'a (uk 73) na alikuwa mwendawazimu.

Mwandishi anaeleza kuwa Kongowea alipata kazi katika karakana ya Abdul Mohammed aliyeishi Tononoka (uk 70). Aidha, maelezo ya mwandishi kumhusu mamake Rashid Omar ni kuwa aliuza mboga katika soko la Mwembe Tayari (uk 71). Rashid mwenyewe alikuwa na mchumba Zawadi aliyekuwa Mbarawa na mwalimu kule Lamu. Zawadi alisomea kozi ya ualimu katika chuo cha Iregi (uk 98). Siku ya uchapaji wa kadi za harusi ya Rashid, Kongowea alitembea naye hadi Kengeleni-makutano ya barabara kuu iendayo Malindi. Ilibidi wavuke daraja la Nyali karibu na hospitali ya Makadara. Baadaye, Rashid alipata ajali karibu na *Bamburi Police Station* (uk 75). Rashid alikuwa amekusudia kusafiri bara-Lodwar, Nairobi na Kisumu kwa fungate yake (uk 76). Ilimbidi Kongowea kumtumia Zawadi barua kuhusu ajali hiyo katika posta iliyopo makutano ya barabara ya Nkrumah Road na Digo Road. Jeneza lililotumiwa lilitegenezwa na Kongowea katika mtaa wa Kibarani na mazishi kufanyika Makaburini karibu na Kisauni (uk 81). Baada ya mazishi, Zawadi alihamishwa katika shule ya Msingi ya Mlaleo (uk 84) mjini Mombasa.

.

Kongowea anasema kwamba alikutana tena na Amina akiwa amebadilika na kuwa hamali, akitoka Mwembe Tayari kununua mboga za kuuza huko Changamwe (uk 79). Katika harakati za kumtafuta babake, Kongowea alipanda gari moshi mjini Mombasa hadi Nairobi. Aliabiri tena gari moshi lililokwenda Malaba mpakani wa Kenya na Uganda (uk 103). Gari la moshi lilimfikisha Eldoret, wilaya ya Uasin Gishu usiku wa manane kisha akapanda gari la kwenda Kitale ambapo alifika saa tatu asubuhi.

Bi Rahma alikuwa amemwambia kuwa babake Juma Mukosi aliishi Makutano kwa Ngozi. Kongowea aliingia katika mkahawa ulioitwa Sidiakhala na kupata chai ya mkandaa (uk 104). Katika mkahawa huu, alihisi kisulisuli kisha akaanza kutapika. Alipelekwa hospitali ya Wilaya ya Trans Nzoia mjini Kitale na Mercy Macdonald (uk 117). Ustadi wake katika lugha ya Kiswahili ulimfanya Kongowea kualikwa na Bi Nambuye Pilipili katika shule ya upili ya Suwerwa ili kutoa mhadhara kuhusu "Matatizo yanayoikabili Lugha ya Kiswahili" (uk 126).

**Uhalisia wa Kimaudhui**

Msanii yeyote yule hutoa maudhui yake katika mazingira ya jamii fulani ambayo yeye ni mhusika kwa namna moja au nyingine. Kazi yake ya fasihi anayoiumba msanii, hutokana na ufahamu wa msanii mwenyewe juu ya maisha na matukio ya jamii hiyo kutokana na kufahamu miktadha anuai ya jamii hiyo. Maudhui huyaumba kulingana na aina ya mipaka ya muktadha wa jamii anayoitungia kazi hiyo ya fasihi. Kauli hii inatiliwa mkazo na Ntarangwi (2004), anayesema kuwa fasihi ina uhusiano na maisha ya kila siku ya jamii kwani haikui (fasihi) wala kuchipuka katika ombwe tupu. Anatoa rai kuwa fasihi hupewa msukumo, umbo, mwelekeo na upeo na nguvu zinazotoka katika jamii. Fasihi huwakilisha uhalisi wa maisha ya kijamii kwa upana wake. Makala haya yanalenga kubainisha uhalisia uliopo wa masuala yaliyozungumziwa na mwandishi katika riwaya ya *Siku Njema*.

**Ubakaji na Ukahaba**

Kulingana na TUKI (2014), ubakaji ni tendo la kumlazimisha mtu afanyiwe asichokubali hasa ngono ilhali ukahaba ni tendo la kufanya ngono nje ya ndoa au uhusiano wa watu mbalimbali na kwa malipo. Kongowea aliposafiri kutoka Tanga hadi Mombasa alipatana na Amina waliyesoma naye huko Tanga School (uk48). Walipofika Mombasa walishuka Mwembe Tayari ambapo Kongowea alikabiliana na mandhari ya wanawake waliovaa mavazi haba na kukalia stuli milangoni huku wakikonyezea macho wanaume waliopita (uk 51). Janajike moja lilidai lipewe Kongowea wafanye ngono naye kwani lilimpenda. Lilijaribu kumkaribia na kumvuta kuelekea chumbani mwake hadi mlangoni. Ilibidi Amina kumvuta Kongowea nyuma naye Shakila akaonya lile janajike (uk 52). Amina alimkaribisha Kongowea katika chumba chake kimoja chenye kitanda kimoja. Wanaume waliendelea kubisha mlango kwake. Kongowea alipoulizia kuhusu kazi waliyoifanya wale wanawake, aliambiwa kuwa ilihusu ukahaba kwani walihitaji pesa. Amina alijaribu hata kuweka maji katika karai ili aoge mbele ya macho ya Kongowea (uk 54).

Amina anamwelezea Kongowea kuwa alizaliwa Dodoma kwani babake alifanya kazi na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mama alimzalia mabinti watano basi wakawa na ugomvi baina yao. Babake Amina alihamishwa kutoka Tanga hadi Kampala. Alimwoa bibi mwingine kisha dadaze Amina wakaandamana naye. Amina alifuatana na mamaye aliyeolewa na jitu lingine. Alipopata mchumba mkenya aliyeitwa Onyango na aliyekuwa mwalimu wa Kiingereza katika shule ya Sekandari kule Dodoma, jitu hilo lilipinga kwa misingi ya ukabila na utaifa (uk 56). Onyango alirudi kwao Ukwala na kuoa huko. Basi siku moja mamake Amina alisafiri kwenda Sumbawanga kumwona kakake na kumwacha na babake wa kambo. Usiku jitu hilo lilimbaka ndiposa maisha yakakosa maana na akaamua kwenda Mombasa kuishi kama kahaba. Hata hivyo, Amina alimwambia Kongowea kuwa hakuipenda kazi hiyo.

Katika ukurasa wa 82, Mabruk anasema kuwa alikwenda danguroni na kuchuma ugonjwa uliosambaratisha afya yake. Awali alikuwa na siha nzuri. Wanapokutana na Amina ansema,
“Sasa ni mwanamke mwenye heshima yake. Hakuna lisilowezekana” (uk 82).
Amina alikuwa kabadilika na kuwa hamali.

**Changamoto katika Ndoa**

Mwandishi amezungumzia ndoa ambazo zilifanyika na zingine ambazo zilikusudiwa.

***Ndoa zilizofanyika***

Mzee Mwinyi Makame alikuwa na wake kumi na wawili na watoto tisini. Makame alipoaga, familia yake ikawa haina chakula, nguo na uhasama wa wake wenza na migogoro ya wake na watoto ilizidi. Mamake Zainabu aliyekuwa mke wa mwisho wa Mzee mwinyi alirejea kijiji cha Chongoleani na hakuolewa tena (uk 1). Alikuwa na watoto watatu; Kitwana, Salim na Zainabu.

Zainabu Makame alimzaa Msanifu Kombo huko Tanga 1957 wakati nyanyake alikuwa keshaaga. Mama alimlea Msanifu Kombo bila baba. Watoto wa Tanga School walikuwa wakimwita mwanaharamu msi baba. Jina baba lilibaki kuwa kitendawili kwa Kongowea (uk 3).

Mjomba Kitwana alimwoa Mwana Saumu. Walibarikiwa na watoto watatu; Rehema, Daniel na Butambo. Saumu hakumpenda Kongowea kwani ingawa watoto wake walimtangulia shule, Kongowea aliwashinda na hata kuwapita basi akawa anamwonea wivu (uk 7). Baada ya Zainabu kufa ilimbidi Kitwana kumchukua Kongowea waishi naye. Hata hivyo, Mwana Saumu alikuwa akimpa Kongowea makombo na kazi nyingi huku binamuze wakikaa starehe na kusoma (uk 23). Pia walimtusi. Kitwana aligonjeka mkono na kufunga karakana yake na kukaa kitandani. Hili lilisababisha Mwana Saumu kulalamika kuwa asingeweza kumlisha Kitwana na Kongowea hadi akaamua kumtilia sumu katika chai iwapo angepita mtihani wa darasa la saba (uk 25). Hata hivyo, Kongowea aliamua kukimbilia Mombasa kwa Mjomba Salim.

Ndoa baina ya wazazi wa Amina ilikabiliwa na changamoto. Mamake Amina alimzalia babake mabinti watano bila mtoto wa kiume. Hili lilizua mgogoro baina yao. Babake alipohamishwa kikazi kutoka Tanga hadi Kampala, alitengana na mamake Amina na kuoa mke mwingine (uk 55).

Mjomba Salimu alimuoa Wamboi kutoka Murang’a lakini ndoa yao haikudumu. Wamboi alipatwa na wendawazimu na mtoto wao Bakari kawa mwizi huku Salim akipotea (uk 65). Mhusika Mercy Macdonald aliolewa na Mzungu Patrick Macdonald. Baada ya kumzaa Alice, Macdonald alifariki katika ajali ya ndege (uk 116).

***Ndoa zilizokusudiwa***

Juma Mukosi alikutana na Zainabu Makame kule Mombasa akitafiti lahaja ya Kimvita. Walichumbiana lakini mahasidi wakamfitini Juma kwa Zainabu akamkataa. Zainabu alikuwa tayari ana mimba ya Kongowea. Baada ya Zainabu kumkataa maisha yalikosa maana (uk 132). Aliamua kujitenga na kuishi mpweke kule Makutano kwa Ngozi mjini Kitale.

Mhusika Amina alikuwa na mchumba Mkenya, Onyango kutoka Ukwala waliyepatana Dodoma. Babake wa kambo alimkataa kwa misingi ya ukabila na utaifa. Onyango aliporudi kwao Ukwala, alioa (uk56). Rashid Omar naye alichumbiana na Zawadi, Mbarawa aliyekuwa mwalimu kule Malindi. Wawili hawa walikusudia kufunga ndoa lakini wazazi wa Zawadi waliipinga kwani Rashid hakuwa na asili wala fasili (uk 71). Hata hivyo, walipanga harusi ambayo haikufanyika kwani Rashid alikufa katika ajali ya gari siku tatu kabla ya harusi yao (uk 76). Zawadi

alidhania kuwa wazee wake walimwendea mpaka kwa waganga ili wasioane kwani walifurahia kufa kwa Rashid na kumzuia kuhudhuria mazishi yake (uk 82). Ilimbidi atoroke kwao. Rashid hakujua asili yake kwani marehemu mamake hakumwambia. Mamake alimzaa Rashid tu.

**Uadilifu**
Kulingana na TUKI (2014), uadilifu ni ile hali ya kuwa muaminifu au kutenda haki bila kupendelea upande wowote. Mwandishi anaeleza jinsi Kongowea alivyompata Selemani na genge la wezi likimpiga hedimasta akiwa uchi na kumjeruhi kichwa. Selemani alimpiga hedimasta kwa kumwamuru aoge mbele ya wanafunzi kisha alimwonya Kongowea kutowasema. Hata hivyo, Kongowea aliwasema ndiposa wakatiwa baroni. Selemani na wenzake walikiri mashtaka na kufungwa kwa miaka miwili na viboko vinne kila mmoja. Selemani aliamua kulipiza kisasi kwa Kongowea atokapo kifungoni (uk 22).

Vumilia alimpa onyo Kongowea kuwa Mwana Saumu na Bi Rahma walikuwa na njama ya kumwangamiza kwa kumtilia chai sumu iwapo angepita mtihani wa darasa la saba (uk 25). Kongowea alipofanya mtihani alikuwa katika safu ya watahiniwa wachache katika nchi nzima ya Tanzania waliopata alama zote. Mjomba Kitwana ingawa mgonjwa alifurahi lakini Mwana Saumu alijifanya tu. Alimpa Kongowea chai iliyotiwa sumu. Kongowea aliikataa basi akatukanwa (uk 26). Hatimaye alitorokea Mombasa.

Vumilia alimfuata Kongowea kwa vyovyote vile ili amwoe. Kongowea anasema kuwa adhuhuri moja akiwa bafuni akitaka kuoga, kaangika nguo zake kwa msumari alijipata kaangaliana ana kwa ana na Vumilia. Alikuwa amesimama wima mlangoni kisha akaziwahi nguo zake. Kongowea aliotama huku Vumilia akimwambia kuwa siku moja angemwoa. Vumilia alimrudishia nguo zake na kumwambia azingatie maneno yake (uk 94).

Kongowea alipofika Mombasa kutoka Tanga usiku, hakuwa na pa kukaa. Amina alimkaribisha katika chumba chake kimoja na kitanda kimoja na kuweka maji ili aoge mbele yake. Alivua nguo na kuoga mle chumbani. Kongowea alifumba macho hadi Amina akamaliza. Baadaye alimwita walale. Hakuona cha kuwazuia. Kwa heshima yake, Kongowea alikataa. Amina alivaa nguo na kwenda kulala na mwanamke mwingine jirani (uk 58-59).

Baada ya mazishi ya Rashid, Kongowea alipoteza fahamu na kulazwa katika hospitali ya Makadara kwa mwezi mmoja. Aliporuhusiwa kwenda nyumbani, Amina na Zawadi walimuuguza kama mtoto mdogo katika chumba chao. Walilala ubavuni pake kitandani kwa zamu (uk 90). Kongowea alipokuwa akiishi na familia ya Mercy Macdonald kule Kitale, Alice aliingia chumbani mwake ghafla kavalia kirinda tu bila sidiria. Alice alimwomba msamaha kwa kumwona kama matapishi na kisha kumwambia kuwa alimpenda *seriously*. Kongowea alimwomba akalale akakataa. Alice aliketi kitandani mwa Kongowea na kuanza kumpapasa. Kongowea alimwambia kuwa amwogopa kisha akainuka kwenda kulala kwenye banda la John Amon (uk 115).

**Matumizi ya Dawa za Kulevya**
Kulingana na TUKI (2014), dawa za kulevya ni kemikali ambazo ziingiapo mwilini huathiri ubongo wa mtumiaji na kumsababishia kuwa na matendo, hisia, fikra na muonekano tofauti na matarajio ya jamii. Selemani alipoogeshwa mbele ya wanafunzi na hedimasta, alijiunga na genge la vijana mjini Tanga. Walivuta bangi, kuiba na kunajisi mabinti za watu (uk 20). Bakari naye alikuwa mwizi na alipigwa kwa kunyakua pochi ya mwanamke mtalii kule Mombasa. Rashid alisema kwamba Bakari alikuwa na uraibu wa bangi na wizi (uk 65). Kulingana na mwandishi, Selemani alimfuata Kongowea kule Mombasa kwa nia ya kulipiza kisasi. Alijiunga na Bakari (uk 103) ili kuwa majambazi. Wawili hawa walishirikiana katika kuvunja mahame ya Salim na kuiba vitu vyote vyenye thamani. Hawakutiwa baroni maana hapakuwa na ushahidi (uk 91). Ilikuwa ni polisi kuwapiga risasi na kuwaua wakijaribu kuiba gari mjini Mombasa. Walikuwa miongoni mwa genge lililowahangaisha wakazi wa mji wa Mombasa kwa muda mrefu (uk 131).

**Mchango katika Lugha ya Kiswahili**
Kulingana na mwandishi, baadhi ya wahusika walichangia katika kuiendeleza lugha ya Kiswahili jambo ambalo lingali linaendelea katika hali halisi ya sasa. Wahusika hao ni kama Zainabu ambaye alimiliki vitabu vya safu ya vitabu vya mashairi ya Kiswahili. Alisoma tungo hizo na kutunga pamoja na kuimba nyimbo za taarab (uk 5). Zainabu alikuwa ashiki wa lugha ya Kiswahili na ushairi. Alimrithisha Kongowea kipawa hicho kwani alipojua kusoma alizipitia tungo za Kiswahili alizopata vitabuni na magazetini. Alihakikisha kwamba Kongowea hahukosa nakala ya magazeti ya *Ngurumo*, *Mapenzi ya Mungu* na *Baraza*.

Kitwana alimpeleka Kongowea Tanga School 1962 mjini Tanga kilicho kitovu cha baadhi ya malenga wa Kiswahili hususan Sheikh Kaluta, Shaaban Robert, Ali Zakwany na Mwalimu Mbega. Malenga hawa walimtia Kongowea hamu ya kukisoma Kiswahili. Mzee Uledi Makali aliyekuwa mtambaji hadithi hodari alimfundisha jinsi ya kuimba mashairi katika mahadhi mbalimbali (uk 6). Kutokana na ari hii, Kongowea alijua Kiswahili zaidi ya wenzake wa hirimu na elimu yake. Aliwahi kutunga hadithi kuhusu kijana aliyemwita Kongowea Mswahili, ilichukua nafasi ya kwanza katika mashindano ya uandishi katika shule mkoani Tanga. Alikuwa darasa la sita. Wenzake walimpagaza jina hilo badala ya Msanifu Kombo. Mamake, Mjomba Kitwana na walimu wake walifaharika. Jina lake lilitokea katika chapa ya magazeti ya Tanzania na kusikika redioni (uk 7). Mara nyingi aliitwa bingwa wa Kiswahili.

Zainabu alipoanza kuugua wakati mwingine alimwomba Kongowea amsomee shairi moja au mawili kwenye *Sauti ya Bara*, diwani aliyoipenda sana. Alipoaga, gazeti la *Baraza* lililochapishwa nchini Kenya liliangazia habari zake. Kongowea alimwomba Vumilia gazeti lenyewe alihifadhi kwani lilikuwa na kitengo cha juu cha lugha (uk 16). Katika safari ya Kongowea kutoka Tanga kwenda Mombasa, mkobani alibeba vitabu vitatu vya Kiswahili: *Shani Kubwa*, *Sauti ya Bara* ya Amuj Isokum na *Kamusi ya Kiswahili* ya F. Johnson aliye kitalii Kiswahili na kuking'amua kuliko Waswahili kwa asili (uk 47). Kongowea anasema kuwa wakati wa kustarehe alitembelea maktaba ya umma Mombasa Kisiwani kusoma vitabu, kuandika mashairi na hadithi fupifupi. Baadhi ya mashairi yake yalitokea katika ukurasa wa mashairi wa magazeti ya *Baraza* na *Taifa Leo.* Alipenda kuchangia utukufu wa lugha ya Kiswahili (uk 74).

Kongowea alipofika Kitale katika hoteli ya Sidiakhala aliwapata watu waliotumia Kiswahili chenye makosa yaliyozoeleka. Waliokitumia hawakuona kwamba walikuwa wakikiuka kanuni ya ufasaha wa kusema na sarufi ya lugha (uk 106). Ufasaha wa kuandika na kuzungumza katika lugha ya Kiswahili haukutiliwa mkazo. Haya yalimkereketa Kongowea. Kongowea alipatana na Alice, mwanafunzi katika shule ya upili ya Suwerwa ambaye hakujua Kiswahili wala kulipenda somo lenyewe. Siku moja Alice na wenzake shuleni walisomewa shairi kutoka katika gazeti la *Baraza*. *Lilikuwa* limetungwa na Kongowea na kuwekwa anwani ya Makutano kwa Ngozi (uk 113). Mwalimu alisifia utunzi ule na kuulizia aliyemjua mtunzi ndiposa Alice akasema kuwa alimjua. Alice alimwomba Kongowea amsaidie kuchambua mashairi ya diwani ya *Sauti ya Bara* ya Amuj Isokum. Hatimaye, mwelekeo wa Alice kukihusu Kiswahili ulibadilika.

Mhusika Kongowea alipokutana na Mwalimu Nambuye alimwambia kuwa ustadi wake wa mashairi ulifanana na wa Amuj Isokum mtunzi ambaye hakujulikana asili yake. Nambuye alimwomba kwenda kuwazungumzia wanafunzi wake kuhusu masuala yoyote ya ushairi ama Kiswahili kwa jumla (uk114). Wakati huo shairi lake Kongowea lilikuwa limepata nafasi ya kwanza katika mashindano ya utunzi wa mashairi nchini Kenya. Kongowea aliitikia wito huo. Alipokuwa njiani kwenda kutoa mhadhara katika sekondari ya Suwerwa alikutana na Mzee Kazikwisha aliyetambua kuwa wazazi wake walimrithisha ukwasi wa lugha.

Katika sekondari ya Suwerwa Kongowea alitoa mhadhara kuhusu "*Matatizo yanayoikabili lugha ya Kiswahili".* Alieleza kuwa alikipenda Kiswahili kama Shaaban Robert na Wazungu kama Sheikh Lambert. Hatimaye alisema kuwa ustawi wa Kiswahili ulitegemea kila mmoja ila wengi hawajifungi nira kukiendeleza.
"Tatizo kubwa sana linaloikumba lugha ya Kiswahili ni wewe na mimi…" (uk 129).
Mhadhara wake ulimvutia Kazikwisha aliyekuja kusikiliza huku amejibanza nje ukutani mwa ukumbi. Alishindwa kwa nini Kongowea hakuwa mtangazaji wa redio kutokana na ufasaha wake wa lugha ya Kiswahili. Mzee Kazikwisha alichangia katika kukiendeleza Kiswahili kwani aliandika diwani ya *Sauti ya Bara* ambayo ilisomwa na wengi. Alikuwa mhadhiri wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Anasema katika barua kwa Kongowea kuwa alikutana na Zainabu kule Mombasa alipokuwa akitafiti lahaja ya Kimvita (uk 132).

**Mabadiliko**
Kulingana na TUKI (2014), kitenzi "badilika" kina maana ya kuwa tofauti na ilivyokuwa mwanzo. Mwandishi amewatumia wahusika ambao wamedhihirisha mabadiliko katika hadithi. Baada ya Mwinyi kuaga, familia yake ilikumbwa na matatizo ya uhaba wa chakula na nguo, uhasama wa wake wenza, matusi ya watoto na kuchaniana nguo (uk 1). Mwandishi anasema kuwa Zainabu alipokuwa mwenye siha nzuri alikuwa mwimbaji wa taarab lakini baada ya kuugua aliacha kuimba ili atafute matibabu. Mwishowe aliaga (uk 13). Inabainika kuwa Mwana Saumu aliungulika baada ya Kongowea kutunga hadithi na kuchukua nafasi ya kwanza katika mashindano ya uandishi wa shule mkoani Tanga. Alitaka wanawe wawe washindi (uk 6). Hata baada ya Zainabu kufa, alimpokea Kongowea kwake shingo upande. Alifanya juu chini kumrithisha Enock Minja mali ya Kongowea lakini Enock akafa katika ajali ya barabarani akielekea Kitale (uk 25). Alijaribu hata kumtilia Kongowea sumu katika chai baada ya kupita

mtihani wa darasa la saba lakini Kongowea akajifanya kutokuwa na hamu. Aliyapanga haya pamoja na Bi Rahma aliyekuwa msiri mkubwa wa hayati Zainabu hadi alipoanza urafiki naye. Ni wazi kwamba Kitwana alikuwa amemwoa mke mbaya kwani Kitwana alipoumia mkono ilimbidi kufunga karakana yake. Mwana Saumu aliyekuwa msusi alidai kuwa hakuwa na pesa za kumnenepesha yeye na Kongowea. Mwishoni mwa hadithi, Mwana Saumu alimsafia nia Kongowea na akawa anamheshimu kwa staha kubwa (uk 135).

Amina alimwambia Kongowea kuwa hakuipendi kazi ya ukahaba. Alijiunga nayo baada ya babake wa kambo kumbaka na maisha kukosa maana. Hata hivyo, baada ya Kongowea kumshauri kuiacha, alianza biashara ya uhamali (uk 56, 78). Mabruk alikuwa mmoja wa wateja wa Amina kwani anasema kuwa awali siha yake ilikuwa nzuri lakini ikabadilika na kuwa mbaya. Hatimaye, kutokana na maelezo ya Zawadi katika barua kwa Kongowea, Mabruk aliaga (uk 119). Majirani wa Salim walimwambia Kongowea kuwa walikisia kuwa kabadilika baada ya mkewe Wamboi kuwa mwendawazimu na mwanawe Bakari kuwa mwizi. Mwandishi anasema kuwa Wamboi alikuwa mwanamke mustaarabu na mwenye fadhili kabla ya akili kumruka (uk 73). Walisema kuwa Bakari aliedekezwa na mamake labda kwa sababu babake alikuwa mpendaraha na hakupatikana nyumbani.

Mhusika Selemani Mapunda alibadilika baada ya kuagizwa na hedimasta kuoga mbele ya umati wa wanafunzi. Alikataa agizo hilo na kutoroka shule Tanga School akawa anazurura ovyoovyo mjini Tanga. Alijiunga na genge la vijana wakawa wanavuta bangi, kuiba mali za watu na kunajisi mabinti za watu (uk 20). Alitoroka gerezani Tanga na kwenda Mombasa ambapo alijiunga na Bakari katika wizi. Hatima yake ilikuwa ni wote wawili kupigwa risasi na polisi mjini Mombasa (uk 131).

Alice anamwambia Kongowea kuwa hakukipenda Kiswahili lakini moyo wa kuchukia ukageuka kukipenda. Haya yalitendeka baada ya Kongowea kumsaidia kuichambua diwani ya mashairi ya *Sauti ya Bara* ya Amuj Isokum (uk 120). Mwelekeo wake kumhusu Kongowea ulibadilika tu alipotambua kuwa Kongowea alikuwa stadi katika lugha ya Kiswahili. Zamani akimwona kama matapishi.

Mwandishi anahitimisha hadithi kwa kusema kuwa:
"Hakuna kitu cha kudumu ila 'mabadiliko' yenyewe" (uk 135).
Anasema pia maoni yake kuhusu ndoa yalibadilika na anapoandika anaiona ndoa kama zawadi kutoka kwa Mungu. Mwandishi ashaamuoa Vumilia, rafikiye wa utotoni. Wako na wana wawili na binti mmoja.

**HITIMISHO**
Makala haya yamebainisha kuwa mwandishi ametumia mandhari ambayo yana uhalisia kwani majina yaliyotumika yanapatikana katika nchi za Afrika Mashariki hususan Uganda, Tanzania na Kenya. Isitoshe, maudhui yaliyoangaziwa yanahusu matukio ya kawaida katika jamii. Kwa hakika, mwandishi ameonyesha uhalisia kwa kuangazia maudhui ambayo jamii inakumbana nayo kila uchao. Ishara kuwa mwandishi aliathiriwa na mazingira yaliyomzunguka kwani kazi yake imechotwa kutoka katika jamii halisi.

**MAREJELEO**


Arthur M, (1918). *Realism: A Study in Art and Thought*. London: Constable and Company Ltd.

Cheruiyot, K. (2020). Ken Walibora: Life and times of renowned author. https://www.the-star.co.ke/news/2020-04-15-ken-walibora-life-and-times-of-renowned-(15 April 2020)

Gikambi, H. (2020), Ken walibora: Jinsi mfalme wa Kiswahili Kenya alivyonipatia msukumo maishani. https://www.bbc.com/swahili/habari-52451539 (28 Aprili 2020).

Hegel, G.W.F (1979*). Introduction to Aesthetics*. Oxford: Clarendon.

Lukacs, G. (1963) *The Meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin Publishers.

Mushumbwa, A. R (2018). Uhusiano wa Fasihi na Jamii katika Mitizamo ya Fasili za Fasihi. Mwanza – Tanzania. http://kiswahihili.blogspot.com/2018/03/uhusiano-wa-fasihi-na-jamii-katika.html (27/7/2020)

Ntarangwi, N. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College, Rock Island, IL 61201

Walibora, K. (1996). *Siku Njema*. Longhorn publishers. Nairobi: Kenya

Walibora, K. (2014) *Nasikia Sauti ya Mama*. Sasa Sema Publishers.Nairobi: Kenya.

Wamitila, K. W (2002). *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wellek, R. (1960). *The Concept of Realism in Literary Scholarship***.** Groningen: J. B. Wolters

TUKI (2014), Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la Tatu. O.U.P. Nairobi. Kenya.


**************